

Pambazuko

Toleo Namba 0037

Jumatatu Mei 08-14, 2023



Habari
Zaidi
Uk. 10

Royal Tour yang'ara

● *Tanapa yahimiza matangazo endelevu*

Serikali yatikisa kiberiti

● *Wabunge waigomea*

Uk.
4

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Nyongeza mishahara ihusishe sekta binafsi

AKIHUTUBIA katika sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) Mjini Morogoro wiki iliyopita, Rais Samia Suluhu Hassan alisema kuwa serikali imeamua kurejesha utaratibu wa kuwaongezea wafanyakazi mishahara yao kila mwaka.

Utaratibu huu ilikuwapo tangu zamani nchini Tanzania na ulikuwepo kwenye sheria, lakini serikali ya awamu ya tano iliisitisha bila kuweka wazi endapo ulifutwa kwa kubadili sheria husika au la.

Wafanyakazi wengi, wakiwamo wa sekta binafsi, baada ya Rais Samia kutangaza kwamba utaratibu wa nyongeza “utarejeshwa” kuanzia mwaka huu, wafanyakazi wamesikika wakieleza kufurahishwa na uamuzi huo wa serikali.

Huu ni utaratibu ambao uliwekwa kuwa motisha kwa wafanyakazi ukiwa ni ziada ya utaratibu mwingine wa kisheria wa kuongeza viwango vya mishahara. Ni utaratibu uliolenga kuwafanya wafanyakazi wajitume zaidi kwani nyongeza hiyo ilitegemea zaidi tija kutokana na utumishi wao.

Suala hili la nyongeza ya mishahara kila mwaka ni tofauti na mabadiliko ya viwango vya mishahara, jambo ambalo linahusu pia sekta binafsi. Suala hilo la viwango vya mishahara pia limeundiwa bodi maalum ambayo ina wajibu wa kutoa mapendekezo serikalini baada ya kufanya utafiti kuhusu viwango vya mishahara.

Bodi hiyo ya mishahara ikishafanya utafiti na kufikisha

mapendekezo yake serikalini na serikali kutangaza viwango vipya vya mishahara, waajiri wote, kutoka sekta ya umma na binafsi, wanalazimika kulitekeleza hilo kwa sababu sheria inawabana kufanya hivyo.

Lakini, hili suala la nyongeza ya mishahara ya kila mwaka, ingawa lilikuwepo kisheria, lilikuwa haliwagusi watumishi wote. Liliwahusu zaidi watumishi wa umma pekee. Nyongeza ya kila mwaka ya mishahara kwa watumishi wa sekta binafsi ilikuwa ni kama fadhila tu.


Kwa maana hiyo, ni wafanyakazi wachache sana kutoka sekta binafsi ambao watanufaika na utaratibu huu uliofufuliwa na Rais Samia. Hii ni kwa sababu waajiri wa sekta binafsi hawabanwi na sheria hiyo ya nyongeza ya kila mwaka ya mishahara.

Hata hivyo, tunampongeza Rais Samia kwa kuona umuhimu wa kulirejesha suala hili kwani lilikuwa ni moja ya malalamiko ya muda mrefu ya watumishi wa umma. Tunaamini kuwa nyongeza hiyo itaongezea motisha ya watumishi na hivyo kuongeza tija.

Lakini, tungeiomba serikali kulirejesha suala hilo kwenye sheria iwapo lilisitishwa kwa mabadiliko ya kisheria. Pia, sheria hiyo itakapohuishwa, basi iwakumbuke pia na watumishi kutoka sekta binafsi na kuwajumuisha.

Hilo likifanyika, ni hakika litaondoa ubaguzi ambao upo kwenye sheria ambayo inawahusu watumishi wa sekta ya umma pekee na kuwacha nje wale wanaotoka sekta binafsi.

ZIARA ...



Rais wa wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan akiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Hosea Kutako, uliopo jijini Windhoek, Namibia jana. Kiongozi huyo wa Tanzania alikwenda nchini humo kwa ajili ya mkutano wa dharura wa wakuu wa Nchi na Serikali za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). (Picha na Ikulu).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



“Mipango mingi ya serikali yetu (Tanzania), inashindwa kuendelea wala kuleta matokeo chanya na makubwa, kwa kuwa kila baada ya muda mfupi, inabadilika ama kuachwa kabisa kwa kuwa kila kiongozi, anayeingia madarakani, anakuwa na matamano yake binafsi na halazimiki kufuata ya mtangulizi wake. Hatufiki bila kuwa na dira itakayosimama bila kujali nani anaingia madarakani”

- Mchungaji Peter Msigwa, mbunge mstaafu.

Habari

Serikali yatikisa kiberiti

Na Mwandishi WETU, Dodoma

SERIKALI imelazimika kuachana na mpango wake wa kufunga shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika kwa kipindi cha miezi mitatu baada ya wabunge “kuja juu” kulipinga suala hilo.

Awali, ilionekana kuwa serikali ilikubaliana na nchi za Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), Zambia na Burundi kusitisha shughuli za uvuvi katika ziwa hilo linaloongoza kwa kuwa na kina kirefu Afrika, kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia katikati ya Mei kama kampeni ya kuongeza idadi ya samaki ziwani humo.

Mjadala mzito ukaibuka wakati Bunge likijadili hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi wiki iliyopita baada ya wabunge kubainisha kuwa kamwe hawawezi kukubaliana na mpango huo kwani utawaathiri watu wengi wanaolitegemea ziwa hilo kuendesha maisha yao.

Wabunge wanaotoka katika mikoa inayopakana na ziwa hilo; Kigoma, Rukwa na Katavi ndiyo waliokuja juu wakipinga mpango huo na kusema kuwa hauna manufaa kwa serikali wala kwa watu wanaoishi karibu na ziwa hilo, hasa wavuvi.

Mbunge wa Kigoma Mjini, Kilumbe Ng'enda (CCM), ambaye katika mchango wake alisema hapingi mpango huo kwa sababu una lengo zuri la kuongeza idadi ya samaki katika ziwa, ingawa akasema namna serikali ilivyofikia uamuzi huo, haikuwa sahihi.

Alisema kuwa hatua ya serikali kutowashirikisha wananchi, hasa wavuvi wanaolitegemea ziwa hilo kwa maisha yao, haikubaliki na yeye haiungi mkono.

Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Aida Khenani (Chadema) alisema yeye hakubaliani na mpango huo kwa sababu utawaumiza wavuvi na watu wengine



Aida Khenani

ambao ziwa hilo ndio msingi wa maisha yao.

“Watu wengi wanategemea Ziwa Tanganyika kuendesha maisha yao kupitia uvuvi na shughuli nyingine, sasa unapolifunga ziwa unataka watu hawa waishi vipi?” alihoji mbunge huyo.

Alisema ni jambo la kushangaza kuwa Tanzania inakubaliana na uamuzi wa kulifunga ziwa hilo na nchi ambazo zinamiliki sehemu ndogo tu ya eneo la ziwa hilo.

Alibainisha kuwa kati ya nchi nne zinazopakana na Ziwa Tanganyika, ni DRC na Tanzania ndizo zinamiliki sehemu kubwa ya ziwa hilo. Akifafanua, alisema kuwa DRC inamiliki asilimia 45 ya ziwa huku Tanzania ikimiliki asilimia 41.

“Hizo asilimia zinazosalia ndizo zinamilikiwa na nchi zilizosalia. Sasa inakuwaje sisi tunakubaliana na nchi ambazo zinamiliki sehemu ndogo tu ya ziwa? Ni dhahiri kuwa watu wetu sisi ndio watathirika sana na uamuzi huo na

Serikali yatikisa kiberiti

Inatoka Uk. 4

mimi sikubaliani nao,” alisema mbunge huyo.

Khenani alisema serikali inalifunga ziwa hilo wakati tayari imeshachukua fedha za wavuvi waliokata leseni za kufanya shughuli za uvuvi kwa kipindi cha mwaka mmoja na kuhoji iwapo wavuvi hao watarejeshwa fedha zao kwa kuwa hawataweza kufanya shughuli zao iwapo kweli ziwa hilo litafungwa.

Mbunge huyo alitaka serikali kulifikiria kwa kina suala hilo na kutokuja na majibu mepesi kwani kulifungia ziwa hilo kuna athari kubwa kwa nchi na wananchi wengi wanaotegemea ziwa hilo kuendesha maisha yao.

Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima alisema uamuzi wa kulifunga Ziwa Tanganyika kwa miezi mitatu ni uamuzi wa kijinga na wala siyo wa kisayansi.

“Tukifunga ziwa hapa kwetu wakati Congo wanaendelea kulitumia ni uamuzi wa kijinga. Wala siyo uamuzi wa kisayansi,” alisema Askofu Gwajima.

Sylvia Francis, ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum (CCM) naye alipingana na uamuzi huo wa serikali akibainisha kuwa hauna manufaa kwa wavuvi na nchi kwa ujumla.

Alisema kuwa uamuzi huo utavuruga kwa kiasi kikubwa uchumi wa maelefu ya wavuvi wanaotegemea Ziwa Tanganyika kuendesha maisha yao na hivyo kuifanya serikali nayo kukosa kiasi kikubwa cha mapato yanayotokana na shughuli za uvuvi.

Kwa upande wake, Mbunge wa Mpanda Vijijini, Selemani Kakoso (CCM) alisema serikali haijafanyia utafiti wa kina kuhusu suala hilo kwani Ziwa Tanganyika hujifunga lenyewe kila mwaka kutokana na jografia yake.

“Tanganyika ni ziwa lenye kina kirefu



Abdallah Ulega

cha maji na kuna kipindi cha miezi kadhaa kila mwaka wavuvi hawapati samaki kwa sababu samaki wote wanakuwa wamekimbilia kwenye kina kirefu ili kukwepa baridi. Hii ina maana kuwa ziwa hilo limejiweka utaratibu wa kujifunga lenyewe kila mwaka, kwa nini serikali ilifunge tena? Alihoji.

Akihitimisha mjadala huo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega aliliambia Bunge kuwa serikali imewasikiliza wabunge na kuamua kusitisha mpango huo.

“Hakuna jambo tunaliheshimu kama kuwaheshimu nyie wabunge mliopigiwa kura na wananchi. Wanasema sauti ya wengi ni sauti ya Mungu. Naomba kuwaeleza wabunge wote wawaeleze wavuvi wa Ziwa Tanganyika waendelea na shughuli zao,” alisema Ulega.

Kutokana na hoja hizo za wabunge, Ulega alisema kuwa wizara yake iliamua kuandaa mkutano na wadau wote wa Ziwa Tanganyika kama sehemu ya ushirikishwaji ambao uliombwa na wawakilishi hao.

Habari

‘Serikali inajenga matabaka’

Na Mwandishi WETU, Dodoma

MBUNGE wa Kigoma Mjini, Kilumbe Ng’enda (CCM), ameionya Serikali kuwa utaratibu wake wa kugawa rasilimali za taifa kupitia miradi ya kimbakati unasababisha matabaka baina ya Watanzania.

Kilumbe, ambaye amewahi kuwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dar es Salaam alitoa tahadhari hiyo wakati akichangia katika mjadala wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Bungeni Jijini Dodoma.

Katika mchango wake, Ng’enda alibainisha kuwa kuna upendeleo katika mgawanyo wa rasilimali za taifa akitoa mifano ya miradi kadhaa ili kuthibitisha hoja yake hiyo.

Alisema kuwa wakati baadhi ya mikoa ikipatiwa rasilimali nyingi kupitia miradi mikubwa inayoitwa ya kimbakati nchini, kuna mikoa ambayo ni kama imesahaulika kwani haipatiwi miradi miradi hiyo au inapata kwa kiasi kidogo.

Aliutaja mmoja wa mikoa anayodai kuwa inapendelewa kwa kumegewa sehemu kubwa ya keki ya taifa kupitia miradi ya kimbakati kuwa ni Mkoa wa Mwanza ambao, kwa maelezo yake, umepatiwa miradi mingi mikubwa huku baadhi ya mikoa kama vile Kigoma, ikiwa imesahaulika katika mgao huo wa miradi mikubwa.

Alisema hivi sasa mkoani Mwanza kuna mradi mikubwa wa ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi linalogharibu zaidi ya Sh. bilioni 700 unaendelea na wakati huohuo mkoa huo umepewa miradi ya ujenzi wa meli mpya na kufanya uwe na meli zipatazo tisa, huku mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) nao ukitekelezwa kwa kasi kuelekea mkoa huo.

Kisha Ng’enda akatoa mfano wa Mkoa wa Kigoma na kubainisha kuwa mkoa huo hauna miradi hiyo mikubwa licha ya mahitaji makubwa ya miradi kama hiyo.

Alibainisha kuwa hata suala la vizimba vya ufugaji wa samaki wa kisasa



Kilumbe Ng’enda

Mwanza imepatiwa vizimba 290 katika Ziwa Viktoria, wakati hakuna kizimba hata kimoja kilichojengwa katika Ziwa Tanganyika mkoani Kigoma.

Ng’enda alionya kuwa suala hilo ni baya kwani linajenga matabaka baina ya wananchi kwani upo uwezekano mkubwa wa mikoa inayopelekewa miradi mikubwa ya kimbakati, kupata maendeleo makubwa baada ya muda, huku wananchi kutoka katika mikoa ambayo “imesahauliwa” wakibakia kwenye lindi la umasikini.

Wakati Ng’enda akitoa mchango wake huo, Mbunge wa Buchosa, Erick Shigongo, alisimama ili kumpa taarifa mbunge mwenzake na kubainisha kuwa daraja la Kigongo – Busisi ambalo ujenzi wake unaendelea, halitatumika na wakazi wa Mkoa wa Mwanza pekee.

“Mathalan, kila siku mabasi takribani tisa yanayoolekea mkoani Kigoma yatapita kwenye daraja hilo litakapokamilika,” alisema.

Hata hivyo, Ng’enda hakukubaliana na taarifa hiyo akieleza kuwa manufaa kwa Mkoa wa Kigoma yatakayotokana na kutumia daraja hilo, ni madogo ikilinganisha na iwapo Kigoma nayo ingekuwa na mradi wenye ukubwa kama huo.

Kabla ya kudai Katiba mpya...

Na Lulu LUSONZO

MIEZI kadhaa iliyopita niliona kipande cha video kikumwonyesha mchora katumi maarufu nchini, Masoud Ally, almaarufu Masudi Kipanya, akitoa maoni yake baada ya kuulizwa msimamo wake kuhusiana na harakati za kudai Katiba mpya.

Kipanya alilijibu swali hilo kwa kuhoji iwapo hao wanaodai katika mpya wataweza kuitekeleza hiyo Katiba wanayoidai wakiipata. Hoja yake ilitokana na kutokutekezwa ipasavyo kwa katiba iliyopo.

Kipanya akahoji iwapo katika iliyopo, ambayo pamoja na upungufu wake katika mambo kadhaa, lakini ina baadhi mambo mazuri, lakini hayatekelezwi ipasavyo, ni vipi Watanzania wataweza kutekeleza hiyo wanayoidai?


Kipanya alimaanisha kuwa kuna umuhimu wa kwanza kuhakikisha Katiba iliyopo inatekelezwa ipasavyo.

Nakubaliana naye kwa sababu iwapo hilo litafanyika tutabaini kuwa kuna mambo mengi ambayo tunayadai yawemo kwenye Katiba mpya ambayo yamo kwenye Katiba ya sasa, lakini kwa sababu hayatekelezwi ipasavyo, basi watu wengi wanadhani mambo hayo hayamo kwenye katiba.

Nimeliangalia suala hilo la Katiba mpya kwa kina baada ya tahariri ya gazeti hili, Pambazuko wiki iliyopita kuweka msisitizo kuwa wakati wa kuandika Katiba mpya ni sasa.

Nakubaliana na msimamo huo, lakini wakati tukishinikiza kupata Katiba mpya tunapaswa pia kuhakikisha kuwa Katiba iliyopo inatekelezwa kikamilifu, hasa kwa yale masuala mazuri yaliyomo ndani yake.

Utekelezaji mzuri wa katiba iliyopo pia utatusaidia kufahamu mashimo yaliyomo kwenye katiba hiyo na hivyo kurahisisha kazi ya kuyatafutia ufumbuzi.



Katiba

Mathalan, watu wanalalamika kuhusu mamlaka makubwa ambayo rais amepewa kupitia katiba hiyo. Hivyo, wanataka katiba ambayo haitarundika mamlaka kwa rais.

Hata Mwalimu Julius Nyerere, muasisi na Rais wa Kwanza wa Tanzania aliwahi kulisema hili kuwa katiba imetoa madaraka makubwa kwa rais na iwapo atatokea mtu mwenye hulka ya kupenda madaraka, basi anaweza kugeuka kuwa dikteta huku akiitumia Katiba kutawala.

Lakini, katiba iliyopo ina vifungu ambavyo vimewekwa kwa ajili ya kudhibiti mamlaka hayo. Tujiulize ni kwa kiasi gani tumetumia vifungu vinavyomdhibiti rais katika matumizi ya mamlaka yake hayo makubwa?

Ileweke kuwa Katiba ya sasa ina kifungu ambacho kinawapa mamlaka

Makala

Kabla ya kudai Katiba mpya...

Inatoka Uk. 7

wabunge kuipigia serikali (inayoongozwa na rais) kura ya kutokuwa na imani nayo.

Iwapo hilo linafanyika, basi rais anakuwa hanabudi isipokuwa kulivunja Bunge na serikali na kuitisha uchaguzi mpya.

Tumeshuhudia nchi ikipita katika kipindi ambacho mambo mengi yaliambiwa na rais, lakini ni lini wabunge walithubutu kutumia mamlaka yao hayo yaliyomo kwenye katiba iliyopo dhidi ya serikali ambayo ililalamikiwa kila uchao kwa kukiuka Katiba?

Katiba iliyopo inatoa mgawanyo mzuri wa mamlaka miongoni mwa mihimili ya utawala; Serikali, Mahakama na Bunge. Lakini tumeshuhudia jinsi mhimili mmoja ukijitutumua na kutaka kujipa mamlaka dhidi ya mihimili mingine. Nani alithubutu kukemea?

Katiba ina vifungu ambavyo vinaelekeza nini kifanyike iwapo mgawanyo huu wa mamlaka ya mihimili utakiukwa, lakini hakuna aliyeinuka kuhakikisha sehemu hiyo ya katiba inatumika kudhibiti ukiukwaji wake.

Ibara ya 20(1) ya Katiba iliyopo sasa inatoa haki ya kuandamana kwa Watanzania, lakini kwa takribani miaka mitano hakuna mtu ambaye aliweza kuitumia sehemu hii ya katiba kutekeleza haki yake kwa sababu tu rais alikuwa amepiga marufuku maandamano.

Hakuna mtu aliinuka kupinga ukiukwaji huo wa Katiba uliofanywa na rais licha ya Katiba kutoa uhuru kwa mtu ambaye anaamini kuwa haki yake imedhulumiwa kuchukua hatua ya kudai haki hiyo.

Sheria zinazokiuka katiba

Hivi karibuni Mahakama Kuu ilitoa hukumu na kueleza kuwa sheria inayoruhusu mtu kutangazwa kuwa



Sheria

mbunge au diwani kwa kile kinachoitwa kupita bila kupingwa ni ukiukwaji wa Katiba ambayo inaeleza kuwa rais, mbunge na diwani watatangazwa kuwa washindi wa nafasi hizo baada ya kupigiwa kura na wananchi.

Sheria hii ya wabunge na madiwani walioshinda bila kupingwa imekuwa ikitumika kwa miaka mingi, lakini kumbe ilikuwa ni kinyume cha Katiba.

Ipo sheria ya ndoa ya mwaka 1971 ambayo inatoa ruhusa kwa mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 14 kuolewa kwa agizo la jaji. Sheria inatoa uhuru wa moja kwa moja kwa mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 15 kuolewa bila haja ya kupata amri ya jaji.

Wapo watu ambao hivi sasa wanafanya harakati za kutaka sheria hiyo irekebishwe ili kufanya umri wa mwanamke kuolewa kuwa zaidi ya miaka 18.

Hili linatokea kana kwamba watu hao hawana habari kuwa ibara ya 20(3) ya Katiba inaeleza kinagaubaga kuwa mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18 ni mtoto.

Kwa maana hiyo, sheria hii inayotoa ruhusa kwa mtoto wa kike wa miaka 14 kuolewa inakiuka Katiba kwa kuruhusu

Endelea Uk. 9

Makala

Kabla ya kudai Katiba mpya...

Inatoka Uk. 7

mtoto aingie katika masuala ya ndoa.

Je, kuna sheria ngapi ambazo ni kinyume cha Katiba iliyopo ambazo zinatumika kwa sababu tu Watanzania hawajaamua kuzihoji mahamani? Tunalaumu Katiba ni mbaya wakati ni sheria, ambazo zinakiuka Katiba, ndizo zinafanya tuione Katiba kuwa ni mbaya.

Hulka za mtu

Wakati Katiba inatoa maelekezo mahsusi kuhusu mgawanyo wa mamlaka katika utawala baina ya mihimili ya Serikali, Bunge na Mahakama, lakini tumeshuhudia mtu, au kundi la watu, kwa hulka zao binafsi wakitoa kauli na kufanya mambo yanayoonyesha kuwa mhimili mmoja una nguvu kuliko mihimili mingine.

Lakini katika uongozi hivi sasa ipo dhana iliyoshika kasi miongoni mwa watumishi wa serikali kuu kuwaona wenzao wa serikali za mitaa kuwa ni dhalili wakati Katiba inatoa mamlaka ya utawala baina ya ngazi hizi za utawala.

Ukiukwaji wa haki

Ibara ya 18 ya Katiba inatoa haki kwa kila mwananchi kutafuta na kusambaza habari. Watu wengi wanadhani haki hii ni kwa ajili ya vyombo vya habari na waandishi wa habari peke yao. La hashah!

Haki hii ni ya kila Mtanzania. Popote alipo raia yeyote wa Tanzania anayo haki ya kupata na sambaza habari na ndio maana zipo sheria zilizotungwa kurahisisha upatikanaji na usambazaji wa habari nchini – ikiwa ni amri ya kikatiba.

Lakini, kinachoshangaza ni kuwa zipo sheria nyingine ambazo zinazuia utekelezaji wa haki hii.

Tumeshuhudia mara kadhaa viongozi wa serikali wakifungia vyombo vya habari na hii inamaanisha kuwa sheria hizo



*Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Tanzania
Elieser Feleshi.*

zinakinzana na Katiba ambayo inatoa haki ya kutafuta, kupata na kusambaza habari.

Pamoja na sheria, pia wapo baadhi ya viongozi katika ngazi mbalimbali ambao kwa utashi wao binafsi, wamekuwa wakizuia utoaji na usambazaji wa habari.

Lakini, pamoja na haki hii inayotolewa na Katiba, baadhi ya watu wameendelea kudai Katiba mpya itakayowapa haki ya kutafuta, kupata na kusambaza habari kana kwamba Katiba ya sasa haitoi haki hiyo.

Kwa ufupi yapo mambo mengi sana ambayo Katiba inayotoa kwa raia, lakini kutokana na kutokuwa na ufahamu nayo, watu wengi wanadhani kuwa mambo hayo hayamo kwenye Katiba.

Ni vyema watu tukajenga utaratibu wa kwanza, kuisoma Katiba na kuelewa vile vilivyomo ndani yake na pili kuhakikisha yale yaliyomo kwenye Katiba yanatekelezwa ipasavyo.

Iwapo tutafanya hivyo, upo uwezekano kuwa madai mengi yanayochangamanishwa na Katiba mpya yakayeyuka kwa sababu yanayodaiwa tayari yamo kwenye Katiba iliyopo.

Habari**Royal Tour yaongeza mapato****Na Mwandishi WETU**

FILAMU iliyotengenezwa kutangaza vivutio vya Tanzania; almaarufu kwa jina la Royal Tour, ikimshirikisha Rais Samia Suluhu Hassan, imedhihirika kuwa kichocheo kuongezeka kwa watalii nchini humo.

Katika kipindi chake cha mwaka mmoja tangu kuzinduliwa, filamu hiyo imekuwa njia rahisi kwa wadau wa utalii wanaofanya biashara ya kutangaza, kushawishi, kusafirisha na kuhudumia watalii kutoka nchi za Italia, Uingereza, Marekani, Ujerumani, Uholanzi na mataifa mengine nje.

Kamishna Mkuu wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), William Mwakilema amesema ubunifu wa filamu hiyo, umesambaa maeneo mengi duniani na kuwa kichocheo cha kuvutia watalii wengi zaidi kutembelea Tanzania.

“Hakika Royal Tour, imekuwa nguzo muhimu kutangaza vivutio vya Tanzania, kwa kipindi cha mwaka mmoja, matokeo yake yameonekana na sasa tunapokea watalii wengi zaidi, hii maana yake ni kuwa na ongezeko kubwa la makusanyo ya fedha zinazotokana na utalii,” amesema Mwakilema.

Mwakilema amesema kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja tangu kuzinduliwa kwa filamu ya “Royal Tour,” jumla ya watalii 259,789 wametembelea Mlima Kilimanjaro na kuliingizia taifa zaidi ya Sh. bilioni 78.

Mhifadhi huyo mkuu amesema kuwa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ilipokea wageni 491,375, na kwamba hii ndiyo hifadhi pekee inayochangia nusu ya mapato yanayokusanywa kutoka katika hifadhi zote zilizoko chini ya Tanapa. Wageni hao waliingiza zaidi ya Sh. bilioni 157 kwa kipindi hicho cha mwaka mmoja.

Mwakilema amebainisha kuwa bado Tanzania ina matumaini makubwa



Rais Samia akishiriki kwenye filamu ya Royal Tour

kwamba filamu hiyo itaendelea kuongeza mapato kwa kupatikana kwa watalii wengi ambao wakipata mwanya wa kuitazama huvutiwa zaidi na utalii ulioko nchini humo.

“Mafanikio haya ya mwaka mmoja, ni makubwa, lakini bado imani ipo kwamba tutapata watalii wengi zaidi, kwani juhudi za balozi za Tanzania nje ya nchi, kwa kushirikiana na wadau wa utalii, zinaendelea kuipaisha na kuhakikisha inawafikia watu wengi zaidi nje ya nchi ili kuwashawishi kuja kutalii Tanzania,” ameongeza Mwakilema.

Ametoa mwito kwa kila Mtanzania kuwa mwakilishi wa kutangaza vivutio vya Tanzania kwani ni jukumu la pamoja; kwa viongozi wakuu, taasisi, balozi, na hata watu binafsi.

“Tanapa inapenda zaidi kusiwepo mipaka ya kuutangaza kwa usahihi utalii wa Tanzania kwa usahihi, ni jukumu la wote kuhakikisha vivutio vyetu vinatangazwa na kusambaa maeneo mengi ya dunia ili vifahamike na kuvutia watalii wengi zaidi,” ameongeza Mwakilema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Utalii ya African Queen Adventures, Alice Manupa, amesema kupitia filamu ya Royal Tour, kampuni yake ilipokea

Royal Tour yaongeza mapato

madaktari 70 kutoka Marekani waliokuja kutembelea vivutio mbalimbali nchini.

Manupa aliendelea kusema kuwa filamu hiyo pia ilichochea utalii wa ndani kiasi cha kuhamasisha wageni wa ndani kutembelea maeneo ya mbuga, hifadhi na milima, ukiwamo Mlima Kilimanjaro.

“Katika kipindi cha mwaka mmoja, jumla ya wanawake 900 kutoka ndani ya nchi walitembelea Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro, mbali na Watanzania wengine waliotembelea eneo hilo,” ameongeza mtendaji huyo mkuu wa liAfrican Queen Adventures.

Katibu Mkuu Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Fatma Mabrouk Khamis amesema kuwa filamu hiyo imeleta manufaa katika sekta ya utalii visiwani humo ikiwa ni pamoja na kuwasili kwa meli nane za kitalii zinazobeba watu 300 hadi 800.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dkt. Hassan Abbas akizungumza kuhusu filamu hiyo, amesema Tanzania imepata manufaa makubwa kutokana na filamu hiyo ya Royal Tour tangu ilipozinduliwa katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

Dkt. Abbas amesema kwamba kati ya Machi 2022 na Machi 2023, mapato ya utalii yaliongezeka hadi kufikia Sh. trilioni 5.8 kutoka Sh. trilioni 3.3 yaliyopatikana

mwaka mmoja kabla ya kuzinduliwa kwa filamu hiyo.

“Filamu hii imeleta manufaa makubwa kwa nchi yetu. Kumekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya watalii, ambapo jumla ya watalii milioni 1.4 walitembelea nchi kati ya Januari na Desemba 2022,” alisema Abbas.

Pia alisema kuwa idadi ya watalii waliorekodiwa ni ongezeko la asilimia 57.7 ikilinganishwa na watalii 620,000 waliotembelea Tanzania mwaka mmoja kabla ya kuzinduliwa kwa filamu hiyo.

Dkt. Abbas alisema kuwa jumla ya watu bilioni 1.2 duniani kote wanaifahamu filamu ya Tanzania Royal Tour kwa kutazama, kusikia au kusoma, hivyo kutangaza utalii wa nchi duniani kote.

Mwaka jana, Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, alizindua filamu ya Royal Tour ambamo yeye mwenyewe ndiye mwenyeji akionyesha vivutio vya utalii wa Tanzania.

Filamu hiyo ya dakika 56 inaonesha vivutio vya utalii vilivyoko Tanzania Bara; Mlima Kilimanjaro, Hifadhi ya Taifa ya Serengenti, na pia maeneo ya vivutio yaliyoko Zanzibar, ambayo ni pamoja na fukwe zenye mchanga mweupe Unguja na Pemba, hoteli ya kitalii iliyoko ndani

Inaendelea Uk. 12



Nyumbu ni kiviutio kikubwa kwa watalii kwa namna wanavyohama kutoka eneo moja kwenda jingine

Habari**Royal Tour yaongeza mapato**

Inatoka Uk. 11

ya bahari huko Pemba.

Katika filamu hiyo, Rais Samia akiwa kiongozi wa filamu hiyo anaonekana akitoa maelezo kuhusu vivutio vingi vya Tanzania na kwamba ushiriki wake unaongeza vionjo na kuvutia zaidi kwa mkuu wa nchi kuwa mwogozaji.

Mwandaaji wa filamu hiyo, Peter Grenberg, ambaye ni mwanahabari nguli na mtunzi wa filamu kutoka kituo cha televisheni cha CNBC nchini Marekani, anaeleza kufurahishwa na namna ushiriki wa Rais Samia ulivyoongeza “vionjo” na kuifanya Royal Tour kuwa moja ya filamu bora alizowahi kuziandaa kutangaza utalii.

Wakati sekta ya utalii inachangia asilimia 17 katika pato la taifa, zaidi ya asilimia 90 ya mapato ya utalii yanategemea wanyamapori. Watalii wengi huja kuwaona tu wanyama, kuwapiga picha na kuondoka.

Tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii inaeleza kuwa wizara hiyo inayo dhamana ya kuhifadhi rasilimali ya wanyamapori nchini na kwamba ili kutekeleza uhifadhi huo, Tanzania imetenga maeneo ya uhifadhi yenye kubwa wa takriban asilimia 28 ya nchi kavu ya Tanzania Bara.

Maeneo hayo yanajumuisha; hifadhi za taifa 16; Hifadhi ya Mamlaka ya

Ngorongoro, mapori ya akiba 28, mapori tengefu 44 na jumuaia za kuhifadhi za wanyamapori 38.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Baraza la Misafara ya Watalii Duniani ya mwaka 2020, nchini Tanzania, sekta ya utalii ni ya pili kuchangia pato la taifa baada ya sekta ya viwanda.

Taarifa hiyo inasema kuwa, mchango wa sekta ya usafiri na utalii katika pato la taifa mwaka 2019 ulikuwa dola za Marekani milioni 6,577.3, sawa na asilimia 10.7 ya pato la taifa.

Taarifa inaongeza kuwa, sekta hii ilizalisha nafasi za kazi 1,550,100 mwaka 2019, ambayo ni sawa na asilimia 11 ya ajira zote nchini Tanzania.

Na kwa mujibu wa Benki ya Dunia (WB), Pato la Taifa la Tanzania liliongezeka kwa asilimia 4.6 mwaka 2022, kutoka asilimia 4.3 mwaka 2021, huku utalii, madini vikitajwa kuchangia ongezeko hilo la makusanyo ya fedha.

Thamani ya pato la taifa kwa bei za sasa ilifikia dola za Kimarekani bilioni 75.5 mwaka 2022.

Pia, takwimu za WB zinaonyesha kuwa pato la taifa lilipanda kwa asilimia 1.4. mwaka 2022 na kiwango cha umaskini kilishuka kwa asilimia 0.3, kwa kutumia viwango vya kimataifa ambavyo vimethibitishwa pia na Shirika la Fedha Duniani (IMF).



Mlima Kilimanjaro

Kifo kuwa hiari kufikia mwaka 2045

Na Mwandishi WETU

MWAKA 2018, wanasayansi wawili wabobezi – wakiitwa wahandisi wa mwili na vinasaba, walizundua kitabu chao Jijini Barcelona, Hispania ambako walikuja na matokeo ya utafiti wao kwamba binadamu anaweza kuishi milele, ikiwa ataamua.

Wataalamu hao wa uchunguzi wa kisayansi kwenye mwili wa binadamu ni Dkt. José Luis Cordeiro wa Venezuela na Dkt. David Wood kutoka Uingereza, ambao katika kitabu chao kilichopewa jina la ‘Kifo cha Kifo,’ wanaeleza kuwa ifikapo mwaka 2045, kufa itakuwa hiari na asiyependa na kuwa na uwezo, basi anaweza kuishi miaka atakayochagua yeye.

Kwamba matokeo ya uchunguzi wao kamwe hauhusishi vifo vinavyotokana na kujinyonga, kupata ajali au kufia vitani.

Wanachozungumza wanasayansi hao ni vifo vinavyotokana na uzee na siyo sababu zingine.

Wengi waliohudhuria hafla hiyo ya uzinduzi wa uchunguzi wao, walionekana kuwa na shaka kuu, wakieleza kuwepo na shaka kubwa ya usahihi wa matokeo yao, lakini kadri muda unavyosonga, wapo wanaoanza kuamini matokeo ya uchunguzi huo wa kisayansi.

Kwamba katika dunia ya sasa ya ukomavu wa sayansi na tiba; vinasaba, seli na nyama za mwili na viungo vingine, ikiwamo moyo, vinaweza kuimarishwa kupitia ‘misuli’ na kufanya viungo hivyo kudumu kwa muda mrefu.

Wanazuoni hao wanabainisha kuwa ni vyema kuanzia sasa uzee ukaainishwa kuwa ni ugonjwa na kwamba unaweza kudhibitiwa kwa kutumia utalaamu wa kisayansi.

Wakitetea hoja zao za matokeo ya uchunguzi, wanasayansi hao wanasema kuwa mchakato wa kuondoa uzee utahusisha kugeuza jeni ‘mbaya’ kuwa zenye afya, kuondoa seli zilizokufa kutoka kwenye mwili, kurekebisha seli zilizoharibiwa, matibabu na seli shina.



David akiwa na Jose wakionyesha kitabu chao kilichoandikwa kwa Kihispania (Picha ya mtandaoni).

Wanasema kwamba kuzeeka ni matokeo ya ‘mikia’ ya DNA, inayojulikana kama ‘telomeres’, katika kromosomu - ambayo kila seli isipokuwa ya damu nyekundu ni fupi, na kuondoa uzee kutahusisha kurefusha hizo telomeres.

Telomeres huharibika na kufupishwa kadiri muda unavyopita, mchakato unaoharakishwa katika tukio la sumu kuingia mwilini - uvutaji sigara, pombe na uchafuzi wa hewa ni miongoni mwa vipengele vinavyopunguza urefu wa telomeres, hivyo kuongeza kasi ya kuzeeka.

Cordeiro na Wood wanaamini kuwa ndani ya miaka 10 ijayo kuanzia sasa, magonjwa yanayohusiana na saratani yatatibika kirahisi kutokana na kukua kwa sayansi ya tiba.

Taarifa za hivi karibuni kuhusu maendeleo ya uchunguzi wao zinaeleza kuwa wameanza kuhusisha watu kadhaa wenye umri mkubwa – kuanzia miaka 70 nchini Columbia, ambako hakuna sheria inayozuia uchunguzi wao.

Inaelezwa na wanasayansi hao kuwa kuna matumaini makubwa ya kuidhahirishia dunia kwamba chunguzi wao hatimaye utahibitika kwa kiwango kikubwa.

Makala haya yameandikwa kwa msaa wa mapitio kadhaa ya kitabu hicho.

Dhana Murua

Wenye sifa hawapatikani kwa bahati

Na Askofu Dkt. Stephen Munga

KATIKA toleo lililopita nilieleza kuwa mtu ni kuwa na sifa za utu. Huyu ni mtu aliyepambwa na vipawa vya asili na vile viitavyo vipawa maalum.

Vipawa hivi ndivyo huonyesha uwezo wa kila mtu kuishi kama yeye binafsi; mvuto na uweleweka wake kwa jamii; na nguvu ya karama zake za utumishi wake kwa jamii na uumbaji kwa jumla.

Kwa hiyo, mtu ni nguvu na uwezo ulioko ndani ya kila mmoja, lakini pia ni jinsi nguvu na uwezo huo unavyoweza kujitokeza kwa namna mtu anavyohusiana na watu wengine (personal and relational).

Uhusiano hapa unachukua dhana pana kuanzia maisha binafsi na wengine kwenye ndoa, familia, shuleni, kazini, michezoni, kwenye uongozi, kwenye kufanya siasa, n.k.


Vilevile nimesema kwamba mtu huyo katika kuishi kwake na kutumia vipawa vyake, anajua kuvitumia na kwa wale wanauguswa na matumizi ya vipawa hivyo. Hapa ndipo hutokeza dhana nyingine ya kuaminika kwa wale anaohusiana nao.

Uzoefu wa upungufu uliyotokea katika maisha ndio umesaidia kuweka sheria ya kuratibisha uwajibikaji - nilitoa mfano wa Torati katika maisha ya Taifa la Israeli.

Katika uhusiano huo kila mtu ana uwezo wa kutambua uwepo wa watu wengine, ukiwemo awezo wa kutambua na kuheshimu haki, uhuru na heshima ya wengine; na wajibu wake kwa wengine na uumbaji wote.

Dhana ya uhusiano na mwingiliano katika kuishi ndio hutupa uelewa wa watu kwamba mtu ni kuthibitika kwa kuwepo wake na utambuzi wa uwepo wa wengine na kukubali hivyo.

Hiyo ieleweke kuwa “watu” siyo watu-watu tu. “Watu” lazima wawekewe



Mwalimu Nyerere, muasisi wa Tanzania.

maelezo (qualified) ili uzito na sababu uwepo wake vionekane. Ieleweke kuwa watu ndio chimbuko la ubora au ubaya wa magurudumu yale mengine mawili – siasa safi na uongozi bora.

Hii ndio sababu kubwa kwamba wajibu mkubwa wa kwanza wa taasisi za jamii ni kufanya maandalizi mazuri ya ‘kuzalisha’ watu bora watakaofanya siasa safi na kuwa viongozi bora.

Hapa taasisi za kijamii ni pamoja na zile zinazojihusisha na uzalishaji, malezi, makuzi, maandalizi, utayarishaji wa watu bora. Kutengeneza watu wazuri ni wajibu wa kwanza wa jamii yeyote yenye maono na malengo chanya juu ya kesho yake.

Watu wenye sifa hizo hawapatikani kwa kubahatisha, bali kwa mipango na malengo ya makusudi. Katika malengo hayo lazima dhamira zitamani kwamba kila kizazi kinachofuata kiwe bora na mahiri kuliko vizazi vilivyotangulia. Pasipo kufanya hivyo, basi ubora wa jamii utaporomoka.

Tangaza na Pambazuko

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.



Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au Barua-
Pepe; info@pambazuko.tz

Uingereza



Jumamosi ya Mei 6, 2023, itabaki kuwa kumbukumbu muhimu kwa historia ya Uingereza (England) baada ya kuapishwa kwa Mfalme Charles III na mkewe, Malkia Camilla. Katika picha hizi zilizopigwa na Chris Jackson wa Kasri la Mfalme, zinaonyesha matukio tofauti ya kutawazwa kwa mfalme huyo, kuwa mkuu wa Uingereza na kiongozi wa Kanisa la Anglikana duniani.



Nguvukazi ni mlango muhimu wa mapato

Na Deusededith KAHANGWA

ADHIMISHO la “Kumbukumbu ya Mei Mosi” limetupa mwanya wa kujadiliana kuhusu rasilimali ya “nguvukazi,” ambayo ni aina mojawapo ya milango ya mapato ya kiuchumi.

Kwa ujumla, katika kila jamii, kuna mapato ya kiuchumi ya aina tano. Kuna ujira unaotokana na kuuza “nguvukazi:” kodi ya pango inayotokana na kuuza au kukodisha ardhii; riba inayotokana na kukodisha fedha; faida inayotokana na kuuza au kukodisha rasilimali ya vitu vinavyotumika kama vitendea kazi; na faida inayotokana na ujasiriamali.

Kwa hiyo, katika kila jamii, kuna rasilimali za aina tano; nguvukazi, ardhii, vitendeakazi, fedha, na ujasiriamali unaohusisha ubunifu na ufundi wa kutumia rasilimali za aina nne za kwanza.

Hivyo, kwa kuzingatia aina tofauti za rasilimali zinazomilikiwa na watu mbalimbali, tunaweza kuwagawanya watu wote katika makundi hayo matano ya wamiliki.

Hivyo, kupendekeza kwamba, baada ya “Sikukuu ya Mei Mosi,” ni wakati wa kutafakari kuhusu uhusiano bora kati ya makundi haya matano ya wamiliki wa rasilimali.

Tafakari hizi zitanoga kama tutakumbuka kwamba, ukubwa wa kipato cha mtu hutegemea mambo mawili; kwanza ni aina na kiwango cha rasilimali anazozimiliki na pili ni bei ya rasilimali hizo sokoni.

Hivyo, kwa upande mmoja, watu wenye kiasi kikubwa cha rasilimali na zenye bei kubwa sokoni, watakuwa na kipato kikubwa. Na kwa upande mwingine, watu wenye kiasi kidogo cha rasilimali na zenye bei kidogo sokoni, watakuwa na kipato kidogo, na hivyo maskini.

Kwa hiyo, tafakari zetu baada ya Sikukuu ya Mei Mosi zinapaswa kutusaidia kujibu maswali mawili



Hii ni ajira rasmi

yafuatayo; kwa nini baadhi ya watu humiliki kiasi kikubwa cha rasilimali? Na kwa nini baadhi ya rasilimali huwa na bei kubwa sokoni kuliko rasilimali baki?

Kuhusu sababu ya baadhi ya watu kumiliki kiasi kikubwa cha rasilimali kuliko wengine, jawabu ni kwamba - ama wamezirithi kutoka kwa wazazi wao au wamezikusanya wenyewe kwa kuweka akiba siku hadi siku.

Na kuhusu sababu za baadhi ya rasilimali kuwa na bei kubwa sokoni kuliko rasilimali baki, kuna majawabu mawili.

Kwanza, kadiri wahitaji wa rasilimali wanavyoongezeka, bei yake hupanda, na kinyume chake ni kweli. Na pili, kadiri wauzaji wa rasilimali wanavyoongezeka, bei hushuka, na kinyume chake ni kweli. Hii ni kanuni ya ugavi na utashi.

Hivyo, tafakari zetu ziendeele kwa kumulika sera za taifa kuhusu uzalishaji na uendelezaji wa rasilimali ya “nguvukazi” iliyo bora.

Yaani, tunapoanza safari ya kuandaa na kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa kuelekea mwaka 2050, yafaa tubainishe sasa mahitaji ya nguvukazi kwa kila sekta na kuwekeza ipasavyo.

Makala**Bado safari ngumu kutengeneza ajira****Na Jumanne KILUSWA**

MANTIKI ya Sikukuu ya Mei Mosi – ya kila mwaka, inavuka mipaka ya wafanyakazi walioajiriwa na kugusa “wafanyakazi walioajiri,” na “wafanyakazi wanaojitolea,” maana wote hawa ni “wafanyakazi” wanaotumia nguvu, akili na muda wao kupata chakula chao kila siku.

Na tunapojadili suala la “wafanyakazi walioajiri” na “wafanyakazi wanaojitolea” yafaa kujielekeza kwenye kundi maalum la vijana.

Kwa mujibu wa takwimu za Baraza la Mitihani la Taifa (Necta), wahitimu wa kidato cha nne wanaopata daraja la kwanza hadi daraja la tatu, hawazidi theluthi moja wa wahitimu wote.

Sera yetu ya elimu na mafunzo inasema kuwa wahitimu waliopata daraja na nne hadi daraja zero hawana sifa ya kujiunga na sekondari, vyyo vya elimu na taasisi za mafunzo ya ufundi katika hatua ya tatu.

Hii maana yake ni kwamba theluthi mbili ya wahitimu wa kidato cha nne hawana sifa ya kujiunga na sekondari, vyyo vya elimu na taasisi za mafunzo ya ufundi katika hatua ya tatu.

Hawa ni vijana wasio katika ajira, elimu wala mafunzo rasmi. Kinyume chake ni kuwepo vijana walio katika ajira, elimu na mafunzo rasmi.

Kwa kawaida hatima ya vijana wasio katika ajira, elimu wala mafunzo rasmi ni kufanya kazi za mikono zilizo katika sekta isiyo rasmi.

Mara nyingi, ni kazi za mitulinga, hazina mikataba rasmi, zinahitaji saa nyingi kuzikamilisha, na zina kipato kidogo, kama tukilinganisha mapato yao na yale ya vijana walio katika ajira, elimu na mafunzo rasmi.

Pamoja na hayo, vijana wasio katika ajira, elimu wala mafunzo rasmi ndio injini ya maisha ya kila siku, kuanzia nyumbani hadi ofisini.

Hawa ndio wapiga rangi, mafundi

*Kazi zisizokuwa rasmi*

bomba, mayaya, mafundi wa simu, mafundi wa luninga, mafundi wa majokofu, madereva wa bodaboda, makonda wa daladala na wakulima wanaotumia jembe la mkono.

Ama ni wafanyakazi walioajiri au wafanyakazi wanaojitolea ambao hawapaswi kuwekwa katika takwimu za ajira rasmi, zinazotambulika.

Takwimu za mwaka 2022 zinaonyesha kwamba ukosefu wa ajira nchini Tanzania ulishuka kutoka asilimia 9.5 mwaka 2020 hadi asilimia 9.3 mwaka uliofuata, 2021.

Kwa kuzingatia mantiki ya kutofautisha vijana wenye elimu na ajira dhidi ya vijana wasiokuwa na elimu wala ujuzi, wanaofanya kazi za kubangaiza, ni wazi kwamba bado tatizo la ajira nchini ni kubwa kuliko kinachosemwa na takwimu hizi.

Kila sekta ya kijamii inahitajika kuweka mikakati ya kuzalisha fursa za kuwapatia nafasi vijana wasio katika ajira, elimu wala mafunzo rasmi ili wapate kipato chao na kisiwe mbali na vijana walio katika ajira, elimu na mafunzo rasmi.



Kashasha aendelea kuenziwa

Na Magadula Kisenha

KITUO cha kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo cha Fountain Gate kilichopo Jiji la Dodoma, kimeongeza hadhi ya mashindano ya kumbukumbu ya mwalimu na mchambuzi wa michezo, hasa soka - Alex Kashasha.

Kituo hicho kimeeleza kwamba kimeamua kuongeza hadhi ya mashindano hayo kwa kualika timu zaidi kutoka nje ya Tanzania kushiriki.

Mashindano hayo ambayo kwa mwaka huu yanaingia msimu wa pili, yanatarajiwa kuwa na timu za vijana kutoka nchi kadhaa za Afrika na Ulaya, ambazo tayari zimepelekewa mialiko na kuonyesha utayari kushiriki.

Mwalimu Kashasha ambaye alikuwa Mkurugenzi wa Ufundi wa Fountain Gate, alifariki dunia Agosti 2021 na anakumbukwa kwa umahiri wake wa kuchambua michezo na wachezaji wa soka wa ndani na nje ya Afrika.

Awali mashindano hayo yalikuwa

yakishirikisha timu za ndani ya Tanzania pekee, lakini sasa yamepandishwa hadhi na kuwa ya kimataifa yakiitwa Kashasha Youth International Tournament.

Mashindano hayo kwa mwaka huu yanatarajiwa kuanza Juni 8 hadi 11 kwenye viwanja tofauti jijini Dodoma, yakishirikisha timu za vijana chini ya miaka 20 Tanzania, nchi za ukanda wa Afrika Mashariki pamoja na mataifa mengine mbalimbali.

Meneja mkazi wa kituo hicho, Calvin Shaban, amesema kutakuwa na mawakala mbalimbali wa ndani na nje ya Tanzania kwa ajili ya kung'amua vijana wenye vipaji.

Miongoni mwa watu wanaotarajiwa kushiriki kuibua vipaji kwa vijana ni pamoja na mchezaji wa zamani wa Liverpool ya England, Alan Nixon.

Mbali na michezo, pia katika siku hizo za mashindano, kutakuwa na semina mbalimbali kuhusu namna bora ya kulinda afya za wachezaji, vyakula na kutambua sheria za soka zitakazotolewa kwa timu zote shiriki.

NEEMA NA CLINTON



Mgombea urais na aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Hillary Clinton, akimsikiliza Mbunge wa Viti Maalum wa Bunge la Tanzania, Neema Lugangira walipokutana New York, Marekani wiki iliyopita katika mkutano wa kimataifa kuzungumzia usawa wa kijinsia. (Picha kutoka mtandao wa Twitter).

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

